# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA TATU

**28 AGOSTI, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA TATU – TAREHE 28 AGOSTI, 2026

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA KILIMO:**

Maelezo ya Waziri wa Kilimo kuhusu Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

**28. MHESHIMIWA EMMANUELA KAGANDA MTATIFIKOLO (ISIMANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatenga fedha za kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Itunundu hadi Izazi yenye Km 45.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**29. MHESHIMIWA REGINA HENRY MIKENZE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwahamisha Watumishi wenye ndoa zinazotambulika Kisheria kukaa karibu na wenza wao.

## OFISI YA RAIS (MAENDELEO YA VIJANA):

**30. MHESHIMIWA MWANAENZI HASSAN SULUHU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana):-

Je, Vijana wangapi wamewezeshwa kupitia programu za uwezeshaji kwa kipindi cha miaka 5 na matokeo yake katika kupunguza tatizo la ajira.

**WIZARA YA AFYA:**

**31. MHESHIMIWA ASMA ALI MWINYI (WELEZO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza huduma za ORCI Mikoani ili kupunguza msongamano wa Wagonjwa katika Hospitali ya *Ocean Road*.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**32. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, Serikali inaweza kufanya majadiliano na Serikali ya China kurahisisha upatikanaji wa VIZA kwa Watanzania wanaofuata bidhaa China.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**33. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga upya Makazi ya Askari Polisi Wilayani Mbulu kwa kuwa yaliyopo ni chakavu.

**34. MHESHIMIWA MOHAMED ABDULRAHMAN MWINYI (CHAMBANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga jengo la Ofisi ya NIDA la Wilaya ya Mkoani katika Mkoa wa Kusini Pemba.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**35. MHESHIMIWA MARY FRANCIS MASANJA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa SGR Dodoma - Mwanza utakamilika ili kurahisisha huduma ya usafiri Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Tabora na Kanda ya Ziwa.

## WIZARA YA MAJI:

### 36. MHESHIMIWA PASCAL LUCAS LUTANDULA (CHATO KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza zoezi la kutoa Maji Buzirayombo na kupeleka Chato Kusini.

### 37. MHESHIMIWA AMINA MUSSA MKUMBA (KIBITI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi wa uchimbaji wa Visima 10 katika Kata ya Kibiti - Jimbo la Kibiti.

## IV. KUTHIBITISHA UTEUZI WA MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:

## V. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **28 AGOSTI, 2026** | **KATIBU WA BUNGE** |